

OFISI YA RAIS – TAMISEMI



TAARIFA KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBER 2021 IKIWA NI ROBO YA KWANZA YA MWAKA WA FEDHA 2021/22

1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inautaratibu wa kutoa Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Mapato ya Ndani kila robo mwaka ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri Nchini. Taarifa hii ni ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 (Kipindi cha Julai hadi Septemba 2021). Aidha, taarifa hii imeandaliwa kwa kutumia Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE).

Taarifa hii inaainisha ufanisi wa kila Halmashauri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kulinganisha makisio yaliyoidhinishwa na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uchambuzi wa matokeo umeandaliwa kwa kulinganisha aina za Halmashauri katika makundi na Kimkoa. Kadhalika, taarifa hii inaonyesha mwenendo wa matumizi ya mapato ya ndani kwa kuainisha matumizi ya Halmashauri kwenye miradi ya maendeleo kwa kuzingatia **asilimia 40 au 60** na **asilimia kumi 10** ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

2.0 MWENENDO WA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI

Kwa mwaka wa fedha 2021/22 Halmashauri zote za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji zilipanga kukusanya **Shilingi Bilioni 863.9** kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani. Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, 2021 Halmashauri zimekusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 212.7** ambayo ni sawa na **asilimia 25** ya makisio ya mwaka sawa na **asilimia 100** ya lengo la robo mwaka. Uchambuzi wa taarifa kuhusu ufanisi wa Halmashauri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, unaonyesha kuwa Halmashauri **5** zimekusanya kwa **asilimia 50** au zaidi ya lengo la Mwaka, Halmashauri **47** zimekusanya kati ya **asilimia 30 hadi 49**, Halmashauri **92** zimekusanya kati ya **asilimia 20 hadi 29**, Halmashauri **37** zimekusanya kati ya **asilimia 10 hadi 19**, na Halmashauri **3** zimekusanya **chini ya asilimia 10**, hii ni kwa kuzingatia lengo la Mwaka. Ulinganisho

wa ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani unaonyesha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya **Hanang** imeongoza katika Halmashauri zote **184** kwa kukusanya **asilimia 66** ya makisio yake ya mwaka, ikifuatiwa na Halmashauri za Wilaya za **Mlele, Ngara** na **Meatu** ambazo zimekusanya **asilimia 51** ya lengo la Mwaka. Hata hivyo, sababu ya Halmashauri hizi kufanya vizuri zaidi katika robo ya kwanza ya mwaka ni kwamba baadhi yao kipindi kizuri cha makusanyo ya mapato ya ndani ni miezi ya Julai hadi Septemba 2021. Aidha, Halmashauri ya **Wilaya ya Tandahimba** imekuwa ya mwisho kwa kukusanya **asilimia 3** ikifuatiwa na Halmashauri ya **Mji Nanyamba asilimia 6** na Halmashauri ya **Wilaya ya Newala asilimia 8**. Sababu ya Halmashauri hizi kuwa na makusanyo ya chini katika robo ya kwanza ya mwaka ni kwamba Halmashauri za Kanda ya Kusini zinategemea zaidi zao la Korosho ambapo msimu wake ni kati ya mwezi Oktoba hadi Disemba. *(Kiambatisho Na. 1A).*

Katika kuzipima Halmashauri zote kwa kigezo cha wingi wa mapato (pato ghafi), Halmashauri ya **Jiji la Dar es Salaam** imekusanya mapato mengi zaidi kuliko Halmashauri zote kwa kukusanya **Shilingi Bilioni 17.8** ikifuatiwa na Halmashauri ya **Manispaa ya Kinondoni Shilingi Bilioni 9.9** na Halmashauri ya **Manispaa ya Temeke Shilingi Bilioni 9.4**. Aidha Halmashauri **6** kati ya 184 zimekusanya kuanzia **Shilingi Bilioni 5** na zaidi *(Kiambatisho Na. 1B)*.

Aidha, **Mkoa wa Manyara** umeongoza kwa kukusanya **asilimia 40** ya lengo la Mwaka, ikifuatiwa na Mkoa wa **Simiyu asilimia 35**, Mkoa wa **Kagera na Songwe asilimia 31** na Mkoa wa **Mtwara** umekua wa mwisho kwa kukusanya **asilimia 12** ukifatiwa na Mkoa wa **Dodoma asilimia 18** na Mkoa wa **Lindi asilimia 20** *(Kiambatisho Na. 2)*.

2.1 TAARIFA YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI KWA KUZINGATIA AINA YA HALMASHAURI

2.1.1 HALMASHAURI ZA MAJJI - Kundi hili linajumuisha Halmashauri 6

Kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Mwaka wa fedha 2021/22 Halmashauri ya **Jiji la Arusha** imeongoza kwa kukusanya mapato kwa **asilimia 27** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na Halmashauri ya **Jiji la Dar es Salaam kwa asilimia 26** na Halmashauri ya **Jiji la Tanga kwa asilimia 25**. Aidha Halmashauri ya **Jiji la Dodoma** imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya **asilimia 16** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na Halmashauri ya **Jiji la Mbeya asilimia 21** na **Jiji la Mwanza asilimia 24** *(Kiambatisho Na. 3A)*.

2.1.2 HALMASHAURI ZA MANISPAA - Kundi hili linajumuisha Halmashauri 20

Kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Mwaka wa fedha 2021/22 **Halmashauri ya Manispaa ya Kahama** imeongoza kwa kukusanya mapato kwa **asilimia 34** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na Halmashauri za **Manispaa ya Bukoba asilimia 32** na **Manispaa ya Mpanda asilimia 29**. Katika kundi hili **Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara** imekuwa ya mwisho ambapo imekusanya **asilimia 15** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na Halmashauri za **Manispaa za Morogoro asilimia 17** na **Ubungo asilimia 18** . (*Kiambatisho Na. 3B*).

2.1.3 HALMASHAURI ZA MIJI - Kundi hili linajumuisha Halmashauri 21

Kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Mwaka wa fedha 2021/22 **Halmashauri ya Mji wa Mbulu** imeongoza kwa kukusanya **asilimia 44** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na Halmashauri za **Miji ya Kibaha asilimia 43** na **Tunduma asilimia 39**. Aidha, **Halmashauri ya Mji wa Nanyamba** imekuwa ya mwisho kwa kukusanya **asilimia 6** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na Halmashauri za Miji za **Newala asilimia 11** na **Halmashauri ya Mji Masasi asilimia 14** (*Kiambatisho Na. 3C*).

2.1.4 HALMASHAURI ZA WILAYA - Kundi hili linajumuisha Halmashauri za Wilaya 137

Kwa kipindi cha robo ya kwanza ya Mwaka wa fedha 2021/22 **Halmashauri ya Wilaya ya Hanang** imeongoza kwa kukusanya **asilimia 66** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na Halmashauri za Wilaya za **Mlele, Ngara, Meatu** kwa **asilimia 51**. Aidha, **Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba** imekuwa ya mwisho katika kundi hili kwa kukusanya **asilimia 3** ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na **Halmashauri ya Wilaya ya Newala** kwa kukusanya **asilimia 8** ya makisio yake ya mwaka (*Kiambatisho Na. 3D*).

3.0 MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI

3.1 MATUMIZI KATIKA MIRADI YA MAENDELEO

Uchambuzi wa taarifa za matumizi ya fedha za mapato ya ndani kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2021 ikiwa ni robo ya kwanza ya Mwaka wa fedha 2021/22 unaonesha kuwa Halmashauri zimetumia **Shilingi Bilioni 47.8** sawa na **asilimia 61** ya fedha zilizopaswa kutumika kwenye miradi ya maendeleo kwa robo ya kwanza ambayo ni **Shilingi Bilioni 78.8** ambazo ni **asilimia 40** kwa **Halmashauri zenye Mapato yasiyolindwa yasiyozidi Shilingi Bilioni 5** au **asilimia 60** ya mapato yalisiyolindwa kwa Halmashauri zenye Mapato yanayozidi Shilingi Bilioni 5. Aidha, **Shilingi Bilioni 165.7** zimekusanywa kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2021 ikiwa ni mapato yasiyolindwa. Halmashauri **14** zimetumia **asilimia 100** au zaidi ya kiasi

kilichopaswa kutumika, Halmashauri **76** zimetumia kati ya **asilimia 50** na **99** ya kiasi kilichopaswa kutumika, Halmashauri **94** zimetumia chini ya **asilimia 50** ya kiasi kilichopaswa kutumika. Aidha taarifa zinaonesha kuwa Halmashauri ya **Wilaya ya Songwe** imeongoza kwa kuchangia **asilimia 190** ikifuatiwa na Halmashauri za **Wilaya za Wanging'ombe asilimia 140** na Halmashauri ya **Wilaya ya Rufiji asilimia 136** Aidha, Halmashauri ya **Wilaya ya Simanjiro** imekua ya mwisho kwa kuchangia **asilimia 1** ikifuatiwa na **Halmashauri za Wilaya za Sikonge asilimia 2, Mkinga asilimia 6 na Halmashauri 9** hazikutumia kiasi chochote cha fedha kwenye miradi ya maendeleo. Halmashauri hizo ni Halmashauri za **Wilaya za Kondoa, Uvinza, Gairo, Tandahimba, Newala, Misungwi, Itigi, Korogwe na Bumbuli** (*Kiambatisho Na. 4*).

3.2 MIKOPO YA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

Uchambuzi wa taarifa za matumizi ya fedha za mapato ya ndani kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba 2021 ikiwa ni robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 unaonesha kuwa Halmashauri zimechangia kiasi cha **Shilingi Bilioni 7.3** kwenda kwenye Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ikiwa ni **asilimia 44** ya kiasi kilichopaswa kuchangiwa kwenye robo ya kwanza ambayo ni **Shilingi Bilioni 16.6** kutokana na **asilimia 10** ya mapato halisi ya vyanzo visivyolindwa kilichokusanywa katika kipindi hicho. Halmashauri **16** zimechangia **asilimia 100** au Zaidi, Halmashauri **54** zimechangia kati ya **asilimia 50 na 99** na Halmashauri **38** zimechangia chini ya **asilimia 50** kwenye mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. Aidha, Halmashauri **76** hazikuchangia kiasi chochote kwenye Mfuko huu. Taarifa zinaonesha kuwa Halmashauri ya **Wilaya ya Mji wa Nanyamba na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala** zimeongoza kwa kuchangia **asilimia 185** ikifuatiwa na Halmashauri ya **Wilaya ya Serengeti asilimia 169**. Aidha, Halmashauri ya **Wilaya ya Simanjiro** imekua ya mwisho kwa kuchangia **asilimia 3** ikifuatiwa na Halmashauri za **Wilaya ya Liwale asilimia 4** na Halmashauri ya **Wilaya ya Kishapu asilimia 13** (*Kiambatisho Na.5*)

4.0 CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA

Tumebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:-

- a) Baadhi ya Halmashauri kutokuingiza taarifa za ukusanyaji mapato lindwa kwenye mfumo wa utoaji taarifa ya mapato na matumizi (FFARS) wa Vituo vya kutolea huduma kwa wakati hivyo, kupelekea ugumu na ucheleweshaji wa uandaaji wa taarifa hii.
- b) Baadhi ya Halmashauri kutumia vifungu visivyo sahihi vya Matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo mfano matumizi yasiyo sahihi kwenye ulipaji wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu, hivyo kusababisha Halmashauri husika kuonekana haijatoa mikopo na kusababisha kutofautiana kwa taarifa kati ya OR – TAMISEMI na Halmashauri.
- c) Baadhi ya Halmashauri kutokufanya usuluhishi (*reconciliation*) wa taarifa za mapato lindwa kwenye mfumo wa Uhasibu wa vituo vya kutolea huduma (FFARS), hivyo kuchelewesha uandaaji wa taarifa kutoka kwenye mfumo.
- d) Baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kufikia malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani, hivyo kuathiri utoaji wa huduma kwa jamii ikiwa ni pamoja na kutokuchangia miradi ya maendeleo na mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.
- e) Mifumo ya utoaji taarifa kutokuwa uwezo wa kutoa taarifa zinazohitajika kulingana na mahitaji. Mfano wa Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) bado una changamoto ya utoaji wa taarifa. Hata hivyo, tunaendelea kufanya mawasiliano na Hazina ili kutatua changamoto hizi.

5.0 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO

- a) Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa zitaendelea kuhakikisha kazi ya uingizaji wa mapato pamoja na usuluhishi wa taarifa za fedha inafanyika kila mwezi ifikapo au kabla ya tarehe 15 baada ya mwezi husika kuisha.
- b) Halmashauri zitaendelea kukumbushwa kuchangia miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mujibu

wa Sheria. Aidha, fedha hizi ziendeleo kutolewa kwenye shughuli zenye tija na zinazogusa Wananchi.

- c) Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa itaendelea kuzisimamia Halmashauri katika masuala ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya mifumo ili kuondoa mianya ya uvujaji wa mapato;
- d) Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.
- e) Ofisi ya Rais-TAMISEMI inazielekeza Halmashauri kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ikiwa ni pamoja na kuwekeza fedha za makusanyo ya ndani kwenye Miradi ya Uwekezaji kama inavyofanyika kwa baadhi ya Halmashauri mfano kwa Manispaa ya Kahama.
- f) Ofisi ya Rais-TAMISEMI inazielekeza Halmashauri kubuni Miradi ya Kilimo cha mazao ya kimkakati (kibiashara) ili kukuza Uchumi wa wananchi pamoja kuongeza makusanyo ya Halmashauri, mfano Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ambayo imeratibu kilimo cha zao la korosho kama sehemu ya zao mkakati.
- g) Ofisi ya Rais-TAMISEMI inazielekeza Halmashauri kuanzisha utaratibu wa kupima ardhi kwa ajili ya mashamba ya ukodishaji ili kurahisisha shughuli za kilimo na hatimaye kuwa na uwakika wa mazao ya chakula na biashara ambapo itaongeza kipato kwa Wananchi na makusanyo ya Halmashauri.
- h) Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa taarifa ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati.

6.0 MAELEKEZO KWA MIKOA, HALMASHAURI ZA MAJIJI, MANISPAA, MIJI, NA HALMASHAURI ZA WILAYA.

(a) Maelekezo kwa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya.

- i) Halmashauri ziimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato ili kuondoa mianya ya uvujaji wa mapato.

- ii) Halmashauri zihakikishe kuwa fedha za makusanyo ya ndani zinazokusanywa kwa kutumia POS na zinapelekwa benki ndani ya masaa 48 badala ya kuzitumia kabla ya kupelekwa Benki.
- iii) Halmashauri zihakikishe zinapeleka **asilimia 40 au 60** ya fedha za makusanyo ya ndani kwenye miradi ya maendeleo ili kutatua kero za Wananchi zinazohusu Elimu, Afya, Miundombinu ya barabara, pamoja na Miundombinu ya kiuchumi na Uwekezaji mfano Masoko na Stendi. Kwa Halmashauri zenye makusanyo kuanzia **Bilioni 5** na zaidi, zihakikishe zinatumia **asilimia 10** ya sehemu ya fedha zao za maendeleo kwenye uboreshaji wa Miundombinu ya barabara kupitia TARURA. Aidha, Wakurugenzi wahakikishe fedha za mapato ya ndani zinatumika kujenga miradi na kukamilika kwa **asilimia 100** ili wananchi waweze kuona faida za mapato ya ndani na hatimaye kuongeza mwamko wa ulipaji wa kodi na ushuru.
- iv) Halmashauri zihakikishe zinakamilisha miradi ambayo haijakamilika (viporo) kabla ya kuanzisha miradi mipya. Ni wajibu wa kila Halmashauri kufanya tathmini ya Miradi ambayo haijakamilika ili kuwekeza nguvu kwenye ukamilishaji wa Miradi hiyo.
- v) Wakurugenzi wa Halmashauri wahakikishe wanapeleka **asilimia 10** ya fedha za mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kama ilivyo idhinishwa kwenye bajeti zao. Fedha hizi zitumike kwenye shughuli zitakazoleta tija kwa Uchumi wa Wananchi na Taifa kwa ujumla.
- vi) Mabaraza ya Madiwani yahakikishe yanasimamia ipasavyo matumizi ya fedha za Halmashauri ili kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika. Hii ni pamoja na kutembelea Miradi yote iliyotekelezwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ili kujiridhisha na matumizi ya fedha hizo kama yanatatua kero za Wananchi.
- vii) Mabaraza ya Madiwani yahakikishe yanajiridhisha na matumizi ya fedha zinazotoka Serikali Kuu, mfano fedha za UVIKO 19, fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya, Miradi ya Elimu, Fedha za EP4R, n.k.
- viii) Halmashauri zihakikishe zinalipa madeni yaliyohakikiwa ya Watumishi, Wazabuni pamoja na Watoa huduma kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za fedha. Pia, ziandae mpangokazi wa ulipaji wa madeni hayo.

(b) Maelekezo kwa Mikoa

- i) Sekretarieti za Mikoa zifanye ufuatiliaji wa mapato na matumizi ya Halmashauri kila robo mwaka ili kujiridhisha na ukusanyaji wa mapato pamoja na matumizi na kuwasilisha taarifa za utekelezaji Ofisi ya Rais - TAMISEMI kabla ya tarehe 20 baada ya robo husika kuisha.
- ii) Sekretarieti za Mikoa zifanye ufuatiliaji wa fedha za miradi iliyopo kwenye Halmashauri zao ili kujiridhisha na ubora wa Miradi inayotekelezwa.
- iii) Sekretarieti za Mikoa zifanye uhakiki wa fedha za mapato ya ndani zilizotumika kwenye Miradi kwenye robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 ili kujiridhisha na Miradi iliyotekelezwa kwa kila Halmashauri na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji Ofisi ya Rais – TAMISEMI kabla ya tarehe 29 Novemba, 2021.
- iv) Sekretarieti za Mikoa zihakikishe zinajiridhisha na matumizi ya fedha zinazotoka Serikali Kuu, mfano fedha za UVIKO 19, fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya, Miradi ya Elimu, Fedha za EP4R, n.k.



Umyy A. Mwalimu (Mb)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS –TAMISEMI

28 Oktoba, 2021

**Kiambatisho Na. 1A: TAARIFA YA MAPATO YA NDANI YA KILA HALMASHAURI KWA MWAKA WA
FEDHA 2021/22 KWA KIGEZO CHA ASILIMIA YA MAKUSANYO KUANZIA MWEZI JULAI 2021
HADI SEPTEMBER 2021 (ROBO YA KWANZA MWAKA 2021/22)**

Na	HALMASHAURI	BAJETI ILIOYODHINISHWA 2021/2022	JUMLA YA MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2021 HADI SEPTEMBER 2021	ASILIMIA YA MAKUSANYO JULAI HADI SEPTEMBER 2021
1	Hanang DC	3,246,000,000.00	2,144,914,817.52	66
2	Mlele DC	957,000,000.00	489,336,954.88	51
3	Ngara DC	2,564,000,000.00	1,302,633,634.92	51
4	Meatu DC	2,574,000,000.00	1,300,749,906.00	51
5	Mpimbwe DC	1,608,000,000.00	801,599,715.72	50
6	Kaliua DC	3,599,000,000.00	1,746,941,247.00	49
7	Mlimba DC	3,367,000,000.00	1,598,667,729.91	47
8	Shinyanga DC	2,294,000,000.00	1,044,410,326.00	46
9	Morogoro DC	3,026,000,000.00	1,364,801,355.18	45
10	Mbulu TC	1,032,000,000.00	450,705,370.97	44
11	Igunga DC	3,267,000,000.00	1,422,282,722.00	44
12	Kibaha TC	4,491,000,000.00	1,927,031,141.39	43
13	Nyang'hwale DC	1,805,000,000.00	758,989,700.27	42
14	Maswa DC	2,252,000,000.00	932,347,098.90	41
15	Rufiji DC	3,657,000,000.00	1,512,847,294.48	41
16	Kiteto DC	2,275,000,000.00	913,756,497.62	40
17	Bariadi DC	1,851,000,000.00	727,744,842.03	39
18	Nsimbo DC	1,191,000,000.00	467,987,996.90	39
19	Mbogwe DC	1,578,000,000.00	617,754,002.00	39
20	Tunduma TC	5,636,000,000.00	2,202,919,681.50	39
21	Momba DC	1,586,000,000.00	589,067,294.92	37
22	Kwimba DC	2,468,000,000.00	911,923,641.51	37
23	Kibaha DC	1,886,000,000.00	695,375,343.05	37
24	Chunya DC	4,847,000,000.00	1,778,054,346.18	37
25	Magu DC	2,505,000,000.00	918,289,501.28	37
26	Mbarali DC	4,790,000,000.00	1,681,365,927.82	35
27	Kongwa DC	3,207,000,000.00	1,114,237,540.40	35
28	Malinyi DC	2,603,000,000.00	895,096,386.42	34
29	Kahama MC	8,325,000,000.00	2,856,363,889.75	34
30	Misenyi DC	3,669,000,000.00	1,242,000,610.50	34

31	Njombe DC	2,982,000,000.00	1,004,868,382.00	34
32	Kyerwa DC	2,653,000,000.00	886,284,814.16	33
33	Mkalama DC	1,454,000,000.00	484,207,243.05	33
34	Mufindi DC	6,130,000,000.00	2,031,931,164.08	33
35	Babati DC	2,935,000,000.00	966,844,041.00	33
36	Muheza DC	2,450,000,000.00	803,954,521.74	33
37	Tarime DC	7,214,000,000.00	2,362,567,662.59	33
38	Karagwe DC	3,326,000,000.00	1,087,702,567.67	33
39	Busokelo DC	1,594,000,000.00	520,477,060.03	33
40	Simanjiro DC	2,473,000,000.00	801,796,633.34	32
41	Bukoba MC	3,200,000,000.00	1,036,065,663.21	32
42	Ulanga DC	2,432,000,000.00	785,981,315.42	32
43	Makete DC	2,487,000,000.00	798,084,493.44	32
44	Biharamulo DC	2,665,000,000.00	853,295,130.44	32
45	Mkinga DC	1,213,000,000.00	384,695,123.34	32
46	Songea DC	1,939,000,000.00	611,731,082.79	32
47	Tarime TC	1,550,000,000.00	488,436,203.00	32
48	Mbozi DC	3,047,000,000.00	941,083,088.00	31
49	Rungwe DC	5,306,000,000.00	1,623,630,850.00	31
50	Uvinza DC	1,942,000,000.00	590,124,110.37	30
51	Mafinga TC	4,965,000,000.00	1,494,452,299.19	30
52	Mbulu DC	1,595,000,000.00	476,481,582.84	30
53	Tabora/Uyui DC	3,007,000,000.00	884,173,423.27	29
54	Geita DC	4,668,000,000.00	1,371,923,346.13	29
55	Njombe TC	6,717,000,000.00	1,970,481,326.80	29
56	Mpanda MC	3,254,000,000.00	949,332,277.17	29
57	Ifakara TC	3,927,000,000.00	1,141,968,833.67	29
58	Ikungi DC	2,192,000,000.00	634,311,298.35	29
59	Kisarawe DC	3,017,000,000.00	870,217,434.22	29
60	Busega DC	2,064,000,000.00	588,578,344.54	29
61	Mkuranga DC	7,826,000,000.00	2,224,978,343.67	28
62	Sumbawanga DC	2,761,000,000.00	781,758,987.30	28
63	Mpwapwa DC	2,237,000,000.00	629,544,453.93	28
64	Urambo DC	2,533,000,000.00	700,151,738.24	28
65	Singida DC	1,357,000,000.00	374,710,837.97	28

66	Itigi DC	1,904,000,000.00	524,969,727.75	28
67	Namtumbo DC	1,501,000,000.00	413,717,593.01	28
68	Kibiti DC	2,107,000,000.00	577,200,092.45	27
69	Kalambo DC	1,856,000,000.00	507,689,402.84	27
70	Mbinga DC	4,091,000,000.00	1,100,465,175.18	27
71	Misungwi DC	2,499,000,000.00	669,124,158.91	27
72	Kondoa TC	1,509,000,000.00	403,082,412.87	27
73	Arusha CC	23,295,000,000.00	6,219,727,850.00	27
74	Ileje DC	1,403,000,000.00	374,451,830.96	27
75	Geita TC	10,254,000,000.00	2,733,828,041.92	27
76	Buhigwe DC	835,000,000.00	220,208,026.71	26
77	Iramba DC	2,429,000,000.00	640,358,877.20	26
78	Ludewa DC	2,037,000,000.00	535,005,378.76	26
79	Bukoba DC	1,863,000,000.00	486,072,684.99	26
80	Singida MC	4,648,000,000.00	1,204,771,058.65	26
81	Longido DC	2,239,000,000.00	580,232,152.59	26
82	Kyela DC	3,884,000,000.00	1,006,392,730.49	26
83	Monduli DC	2,250,000,000.00	581,353,672.43	26
84	Kasulu TC	2,097,000,000.00	538,293,114.00	26
85	Mbinga TC	1,931,000,000.00	493,920,906.17	26
86	Kigoma DC	719,000,000.00	183,686,131.50	26
87	DAR ES SALAAM CC	69,655,000,000.00	17,774,288,777.52	26
88	Babati TC	2,225,000,000.00	563,839,822.00	25
89	Bariadi TC	3,324,000,000.00	830,603,919.84	25
90	Msalala DC	4,608,000,000.00	1,151,167,714.23	25
91	Gairo DC	1,220,000,000.00	303,930,896.50	25
92	Songea MC	4,329,000,000.00	1,077,980,844.04	25
93	Bahi DC	1,700,000,000.00	422,577,772.26	25
94	Temeke MC	37,713,000,000.00	9,371,180,325.00	25
95	Ushetu DC	3,071,000,000.00	762,757,965.60	25
96	Moshi DC	3,898,000,000.00	963,386,035.45	25
97	Kilwa DC	5,500,000,000.00	1,358,437,560.61	25
98	Tabora MC	5,085,000,000.00	1,255,396,328.19	25
99	Itilima DC	1,487,000,000.00	366,404,784.66	25
100	Tanga CC	15,955,000,000.00	3,930,730,365.67	25

101	Chamwino DC	2,106,000,000.00	518,618,480.12	25
102	Bunda TC	1,459,000,000.00	358,975,887.59	25
103	Karatu DC	3,964,000,000.00	975,269,892.58	25
104	Meru DC	3,499,000,000.00	849,077,932.74	24
105	Ilemela MC	9,646,000,000.00	2,335,209,196.19	24
106	Makambako TC	3,228,000,000.00	781,318,648.31	24
107	Iringa DC	3,882,000,000.00	935,126,214.13	24
108	Handeni DC	2,134,000,000.00	512,297,797.30	24
109	Iringa MC	4,357,000,000.00	1,038,049,823.73	24
110	Mwanza CC	17,716,000,000.00	4,199,227,621.69	24
111	Chalinze DC	10,728,000,000.00	2,540,376,723.33	24
112	Bagamoyo DC	3,914,000,000.00	921,454,248.13	24
113	Musoma MC	2,939,000,000.00	691,727,622.25	24
114	Nzega DC	2,567,000,000.00	603,319,868.80	24
115	Sikonge DC	3,229,000,000.00	758,586,238.21	23
116	Kigamboni MC	9,106,000,000.00	2,131,549,642.80	23
117	Shinyanga MC	4,043,000,000.00	938,410,529.34	23
118	Mafia DC	1,680,000,000.00	381,737,064.50	23
119	Kakonko DC	1,039,000,000.00	235,882,234.00	23
120	Mwanga DC	5,066,000,000.00	1,143,483,089.68	23
121	Sumbawanga MC	2,275,000,000.00	510,649,229.25	22
122	Kilolo DC	4,353,000,000.00	976,904,823.00	22
123	Kilosa DC	5,240,000,000.00	1,170,944,996.36	22
124	Rombo DC	2,441,000,000.00	540,485,038.68	22
125	Nkasi DC	2,744,000,000.00	604,042,909.00	22
126	Moshi MC	6,460,000,000.00	1,417,961,546.48	22
127	Wanging'ombe DC	3,489,000,000.00	763,406,131.82	22
128	Lushoto DC	2,514,000,000.00	542,699,283.50	22
129	Handeni TC	1,650,000,000.00	352,374,450.48	21
130	Kibondo DC	2,705,000,000.00	570,823,078.80	21
131	Musoma DC	1,750,000,000.00	368,110,699.74	21
132	Mbeya DC	4,373,000,000.00	915,742,754.48	21
133	Sengerema DC	2,500,000,000.00	523,296,588.49	21
134	Butiama DC	1,545,000,000.00	322,114,280.29	21
135	Mbeya CC	16,610,000,000.00	3,413,533,430.46	21

136	Arusha DC	4,383,000,000.00	900,210,236.80	21
137	Nyasa DC	1,238,000,000.00	251,697,783.53	20
138	Hai DC	3,787,000,000.00	764,042,564.11	20
139	Ruangwa DC	4,961,000,000.00	995,168,214.34	20
140	Kinondoni MC	49,414,000,000.00	9,860,146,626.30	20
141	Lindi MC	2,850,000,000.00	566,689,137.55	20
142	Same DC	2,589,000,000.00	510,272,976.57	20
143	Nachingwea DC	4,002,000,000.00	786,759,048.39	20
144	Tunduru DC	4,278,000,000.00	840,553,237.86	20
145	Muleba DC	5,761,000,000.00	1,119,675,092.25	19
146	Tanganyika DC	5,565,000,000.00	1,069,157,262.98	19
147	Mtwara DC	2,835,000,000.00	543,810,750.46	19
148	Kishapu DC	3,652,000,000.00	696,617,608.47	19
149	Kigoma MC	3,000,000,000.00	563,773,044.00	19
150	Korogwe TC	2,154,000,000.00	403,061,216.98	19
151	Kondoa DC	1,547,000,000.00	288,104,231.00	19
152	Nzega TC	3,673,000,000.00	683,176,540.99	19
153	Chemba DC	1,640,000,000.00	303,478,279.99	19
154	Liwale DC	3,854,000,000.00	700,897,977.66	18
155	Ubungo MC	27,670,000,000.00	5,017,308,060.00	18
156	Manyoni DC	2,897,000,000.00	523,687,043.70	18
157	Nanyumbu DC	2,351,000,000.00	412,714,700.58	18
158	Chato DC	3,996,000,000.00	692,418,666.00	17
159	Madaba DC	1,023,000,000.00	172,480,780.58	17
160	Morogoro MC	11,504,000,000.00	1,926,510,355.14	17
161	Korogwe DC	2,119,000,000.00	351,309,673.58	17
162	Mvomero DC	3,596,000,000.00	588,099,396.13	16
163	Rorya DC	1,380,000,000.00	223,855,309.31	16
164	Siha DC	1,532,000,000.00	244,556,723.93	16
165	Buchosa DC	2,849,000,000.00	450,133,346.67	16
166	Dodoma CC	50,116,000,000.00	7,778,980,401.88	16
167	Ukerewe DC	3,270,000,000.00	500,941,038.51	15
168	Pangani DC	1,770,000,000.00	262,785,417.00	15
169	Songwe DC	3,150,000,000.00	464,805,666.00	15
170	Mtwara MC	4,950,000,000.00	725,172,751.68	15

171	Bukombe DC	3,162,000,000.00	461,520,481.00	15
172	Masasi TC	2,376,000,000.00	330,576,849.67	14
173	Kilindi DC	2,434,000,000.00	337,492,680.99	14
174	Masasi DC	3,480,000,000.00	474,519,195.72	14
175	Bunda DC	1,776,000,000.00	235,608,617.20	13
176	Ngorongoro DC	2,753,000,000.00	362,015,925.00	13
177	Bumbuli DC	1,033,000,000.00	132,274,254.53	13
178	Kasulu DC	2,892,000,000.00	336,344,882.99	12
179	Newala TC	2,212,000,000.00	245,798,704.78	11
180	Serengeti DC	3,558,000,000.00	364,136,541.00	10
181	Mtama DC	2,744,000,000.00	265,062,448.00	10
182	Newala DC	1,638,000,000.00	127,037,880.53	8
183	Nanyamba TC	2,051,000,000.00	123,827,854.88	6
184	Tandahimba DC	5,053,000,000.00	164,617,842.27	3
	JUMLA KUU	863,858,000,000.00	212,680,929,640.66	25

Kiambatisho Na. 1B: TAARIFA YA MAPATO YA NDANI YA KILA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 KWA KIGEZO CHA WINGI WA MAKUSANYO KUANZIA MWEZI JULAI 2021 HADI SEPTEMBER 2021 (ROBO YA KWANZA MWAKA 2021/22)

Na	HALMASHAURI	BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2021/2022	JUMLA YA MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2021 HADI SEPTEMBER 2021	ASILIMIA YA MAKUSANYO JULAI HADI SEPTEMBER 2021
1	DAR ES SALAAM C	69,655,000,000	17,774,288,778	26
2	Kinondoni MC	49,414,000,000	9,860,146,626	20
3	Temeke MC	37,713,000,000	9,371,180,325	25
4	Dodoma CC	50,116,000,000	7,778,980,402	16
5	Arusha CC	23,295,000,000	6,219,727,850	27
6	Ubungo MC	27,670,000,000	5,017,308,060	18
7	Mwanza CC	17,716,000,000	4,199,227,622	24
8	Tanga CC	15,955,000,000	3,930,730,366	25
9	Mbeya CC	16,610,000,000	3,413,533,430	21
10	Kahama MC	8,325,000,000	2,856,363,890	34
11	Geita TC	10,254,000,000	2,733,828,042	27
12	Chalinze DC	10,728,000,000	2,540,376,723	24
13	Tarime DC	7,214,000,000	2,362,567,663	33
14	Ilemela MC	9,646,000,000	2,335,209,196	24
15	Mkuranga DC	7,826,000,000	2,224,978,344	28
16	Tunduma TC	5,636,000,000	2,202,919,682	39
17	Hanang DC	3,246,000,000	2,144,914,818	66
18	Kigamboni MC	9,106,000,000	2,131,549,643	23
19	Mufindi DC	6,130,000,000	2,031,931,164	33
20	Njombe TC	6,717,000,000	1,970,481,327	29
21	Kibaha TC	4,491,000,000	1,927,031,141	43
22	Morogoro MC	11,504,000,000	1,926,510,355	17
23	Chunya DC	4,847,000,000	1,778,054,346	37
24	Kaliua DC	3,599,000,000	1,746,941,247	49
25	Mbarali DC	4,790,000,000	1,681,365,928	35
26	Rungwe DC	5,306,000,000	1,623,630,850	31
27	Mlimba DC	3,367,000,000	1,598,667,730	47
28	Rufiji DC	3,657,000,000	1,512,847,294	41
29	Mafinga TC	4,965,000,000	1,494,452,299	30

30	Igunga DC	3,267,000,000	1,422,282,722	44
31	Moshi MC	6,460,000,000	1,417,961,546	22
32	Geita DC	4,668,000,000	1,371,923,346	29
33	Morogoro DC	3,026,000,000	1,364,801,355	45
34	Kilwa DC	5,500,000,000	1,358,437,561	25
35	Ngara DC	2,564,000,000	1,302,633,635	51
36	Meatu DC	2,574,000,000	1,300,749,906	51
37	Tabora MC	5,085,000,000	1,255,396,328	25
38	Misenyi DC	3,669,000,000	1,242,000,611	34
39	Singida MC	4,648,000,000	1,204,771,059	26
40	Kilosa DC	5,240,000,000	1,170,944,996	22
41	Msalala DC	4,608,000,000	1,151,167,714	25
42	Mwanga DC	5,066,000,000	1,143,483,090	23
43	Ifakara TC	3,927,000,000	1,141,968,834	29
44	Muleba DC	5,761,000,000	1,119,675,092	19
45	Kongwa DC	3,207,000,000	1,114,237,540	35
46	Mbinga DC	4,091,000,000	1,100,465,175	27
47	Karagwe DC	3,326,000,000	1,087,702,568	33
48	Songea MC	4,329,000,000	1,077,980,844	25
49	Tanganyika DC	5,565,000,000	1,069,157,263	19
50	Shinyanga DC	2,294,000,000	1,044,410,326	46
51	Iringa MC	4,357,000,000	1,038,049,824	24
52	Bukoba MC	3,200,000,000	1,036,065,663	32
53	Kyela DC	3,884,000,000	1,006,392,730	26
54	Njombe DC	2,982,000,000	1,004,868,382	34
55	Ruangwa DC	4,961,000,000	995,168,214	20
56	Kilolo DC	4,353,000,000	976,904,823	22
57	Karatu DC	3,964,000,000	975,269,893	25
58	Babati DC	2,935,000,000	966,844,041	33
59	Moshi DC	3,898,000,000	963,386,035	25
60	Mpanda MC	3,254,000,000	949,332,277	29
61	Mbozi DC	3,047,000,000	941,083,088	31
62	Shinyanga MC	4,043,000,000	938,410,529	23
63	Iringa DC	3,882,000,000	935,126,214	24
64	Maswa DC	2,252,000,000	932,347,099	41

65	Bagamoyo DC	3,914,000,000	921,454,248	24
66	Magu DC	2,505,000,000	918,289,501	37
67	Mbeya DC	4,373,000,000	915,742,754	21
68	Kiteto DC	2,275,000,000	913,756,498	40
69	Kwimba DC	2,468,000,000	911,923,642	37
70	Arusha DC	4,383,000,000	900,210,237	21
71	Malinyi DC	2,603,000,000	895,096,386	34
72	Kyerwa DC	2,653,000,000	886,284,814	33
73	Tabora/Uyui DC	3,007,000,000	884,173,423	29
74	Kisarawe DC	3,017,000,000	870,217,434	29
75	Biharamulo DC	2,665,000,000	853,295,130	32
76	Meru DC	3,499,000,000	849,077,933	24
77	Tunduru DC	4,278,000,000	840,553,238	20
78	Bariadi TC	3,324,000,000	830,603,920	25
79	Muheza DC	2,450,000,000	803,954,522	33
80	Simanjiro DC	2,473,000,000	801,796,633	32
81	Mpimbwe DC	1,608,000,000	801,599,716	50
82	Makete DC	2,487,000,000	798,084,493	32
83	Nachingwea DC	4,002,000,000	786,759,048	20
84	Ulanga DC	2,432,000,000	785,981,315	32
85	Sumbawanga DC	2,761,000,000	781,758,987	28
86	Makambako TC	3,228,000,000	781,318,648	24
87	Hai DC	3,787,000,000	764,042,564	20
88	Wanging'ombe D	3,489,000,000	763,406,132	22
89	Ushetu DC	3,071,000,000	762,757,966	25
90	Nyang'hwale DC	1,805,000,000	758,989,700	42
91	Sikonge DC	3,229,000,000	758,586,238	23
92	Bariadi DC	1,851,000,000	727,744,842	39
93	Mtwara MC	4,950,000,000	725,172,752	15
94	Liwale DC	3,854,000,000	700,897,978	18
95	Urambo DC	2,533,000,000	700,151,738	28
96	Kishapu DC	3,652,000,000	696,617,608	19
97	Kibaha DC	1,886,000,000	695,375,343	37
98	Chato DC	3,996,000,000	692,418,666	17
99	Musoma MC	2,939,000,000	691,727,622	24

100	Nzega TC	3,673,000,000	683,176,541	19
101	Misungwi DC	2,499,000,000	669,124,159	27
102	Iramba DC	2,429,000,000	640,358,877	26
103	Ikungi DC	2,192,000,000	634,311,298	29
104	Mpwapwa DC	2,237,000,000	629,544,454	28
105	Mbogwe DC	1,578,000,000	617,754,002	39
106	Songea DC	1,939,000,000	611,731,083	32
107	Nkasi DC	2,744,000,000	604,042,909	22
108	Nzega DC	2,567,000,000	603,319,869	24
109	Uvinza DC	1,942,000,000	590,124,110	30
110	Momba DC	1,586,000,000	589,067,295	37
111	Busega DC	2,064,000,000	588,578,345	29
112	Mvomero DC	3,596,000,000	588,099,396	16
113	Monduli DC	2,250,000,000	581,353,672	26
114	Longido DC	2,239,000,000	580,232,153	26
115	Kibiti DC	2,107,000,000	577,200,092	27
116	Kibondo DC	2,705,000,000	570,823,079	21
117	Lindi MC	2,850,000,000	566,689,138	20
118	Babati TC	2,225,000,000	563,839,822	25
119	Kigoma MC	3,000,000,000	563,773,044	19
120	Mtwara DC	2,835,000,000	543,810,750	19
121	Lushoto DC	2,514,000,000	542,699,284	22
122	Rombo DC	2,441,000,000	540,485,039	22
123	Kasulu TC	2,097,000,000	538,293,114	26
124	Ludewa DC	2,037,000,000	535,005,379	26
125	Itigi DC	1,904,000,000	524,969,728	28
126	Manyoni DC	2,897,000,000	523,687,044	18
127	Sengerema DC	2,500,000,000	523,296,588	21
128	Busokelo DC	1,594,000,000	520,477,060	33
129	Chamwino DC	2,106,000,000	518,618,480	25
130	Handeni DC	2,134,000,000	512,297,797	24
131	Sumbawanga MC	2,275,000,000	510,649,229	22
132	Same DC	2,589,000,000	510,272,977	20
133	Kalambo DC	1,856,000,000	507,689,403	27
134	Ukerewe DC	3,270,000,000	500,941,039	15

135	Mbinga TC	1,931,000,000	493,920,906	26
136	Mlele DC	957,000,000	489,336,955	51
137	Tarime TC	1,550,000,000	488,436,203	32
138	Bukoba DC	1,863,000,000	486,072,685	26
139	Mkalama DC	1,454,000,000	484,207,243	33
140	Mbulu DC	1,595,000,000	476,481,583	30
141	Masasi DC	3,480,000,000	474,519,196	14
142	Nsimbo DC	1,191,000,000	467,987,997	39
143	Songwe DC	3,150,000,000	464,805,666	15
144	Bukombe DC	3,162,000,000	461,520,481	15
145	Mbulu TC	1,032,000,000	450,705,371	44
146	Buchosa DC	2,849,000,000	450,133,347	16
147	Bahi DC	1,700,000,000	422,577,772	25
148	Namtumbo DC	1,501,000,000	413,717,593	28
149	Nanyumbu DC	2,351,000,000	412,714,701	18
150	Kondoa TC	1,509,000,000	403,082,413	27
151	Korogwe TC	2,154,000,000	403,061,217	19
152	Mkinga DC	1,213,000,000	384,695,123	32
153	Mafia DC	1,680,000,000	381,737,065	23
154	Singida DC	1,357,000,000	374,710,838	28
155	Ileje DC	1,403,000,000	374,451,831	27
156	Musoma DC	1,750,000,000	368,110,700	21
157	Itilima DC	1,487,000,000	366,404,785	25
158	Serengeti DC	3,558,000,000	364,136,541	10
159	Ngorongoro DC	2,753,000,000	362,015,925	13
160	Bunda TC	1,459,000,000	358,975,888	25
161	Handeni TC	1,650,000,000	352,374,450	21
162	Korogwe DC	2,119,000,000	351,309,674	17
163	Kilindi DC	2,434,000,000	337,492,681	14
164	Kasulu DC	2,892,000,000	336,344,883	12
165	Masasi TC	2,376,000,000	330,576,850	14
166	Butiama DC	1,545,000,000	322,114,280	21
167	Gairo DC	1,220,000,000	303,930,897	25
168	Chemba DC	1,640,000,000	303,478,280	19
169	Kondoa DC	1,547,000,000	288,104,231	19

170	Mtama DC	2,744,000,000	265,062,448	10
171	Pangani DC	1,770,000,000	262,785,417	15
172	Nyasa DC	1,238,000,000	251,697,784	20
173	Newala TC	2,212,000,000	245,798,705	11
174	Siha DC	1,532,000,000	244,556,724	16
175	Kakonko DC	1,039,000,000	235,882,234	23
176	Bunda DC	1,776,000,000	235,608,617	13
177	Rorya DC	1,380,000,000	223,855,309	16
178	Buhigwe DC	835,000,000	220,208,027	26
179	Kigoma DC	719,000,000	183,686,132	26
180	Madaba DC	1,023,000,000	172,480,781	17
181	Tandahimba DC	5,053,000,000	164,617,842	3
182	Bumbuli DC	1,033,000,000	132,274,255	13
183	Newala DC	1,638,000,000	127,037,881	8
184	Nanyamba TC	2,051,000,000	123,827,855	6
	JUMLA KUU	863,858,000,000	212,680,929,641	25

Kiambatisho Na. 2: TAARIFA YA MAPATO YA NDANI YA KILA MKOA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 KWA KIGEZO CHA ASILIMIA YA MAKUSANYO KUANZIA MWEZI JULAI 2021 HADI SEPTEMBER 2021 (ROBO YA KWANZA MWAKA 2021/22)

Na	MKOA		BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2021/2022	JUMLA YA MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2021 HADI SEPTEMBER 2021	ASILIMIA YA MAKUSANYO JULAI HADI SEPTEMBER 2021	
1	Manyara	1	Simanjiro DC	2,473,000,000	801,796,633.34	32
		2	Mbulu TC	1,032,000,000	450,705,370.97	44
		3	Mbulu DC	1,595,000,000	476,481,582.84	30
		4	Kiteto DC	2,275,000,000	913,756,497.62	40
		5	Hanang DC	3,246,000,000	2,144,914,817.52	66
		6	Babati TC	2,225,000,000	563,839,822.00	25
		7	Babati DC	2,935,000,000	966,844,041.00	33
			Jumla Ndogo	15,781,000,000	6,318,338,765.29	40
2	Simiyu	1	Meatu DC	2,574,000,000	1,300,749,906.00	51
		2	Maswa DC	2,252,000,000	932,347,098.90	41
		3	Itilima DC	1,487,000,000	366,404,784.66	25
		4	Busega DC	2,064,000,000	588,578,344.54	29
		5	Bariadi TC	3,324,000,000	830,603,919.84	25
		6	Bariadi DC	1,851,000,000	727,744,842.03	39
			Jumla Ndogo	13,552,000,000	4,746,428,895.97	35
3	Kagera	1	Ngara DC	2,564,000,000.00	1,302,633,634.92	51
		2	Muleba DC	5,761,000,000.00	1,119,675,092.25	19
		3	Misenyi DC	3,669,000,000.00	1,242,000,610.50	34
		4	Kyerwa DC	2,653,000,000.00	886,284,814.16	33
		5	Karagwe DC	3,326,000,000.00	1,087,702,567.67	33
		6	Bukoba MC	3,200,000,000.00	1,036,065,663.21	32
		7	Bukoba DC	1,863,000,000.00	486,072,684.99	26
		8	Biharamulo DC	2,665,000,000.00	853,295,130.44	32
			Jumla Ndogo	25,701,000,000	8,013,730,198.14	31
4	Songwe	1	Tunduma TC	5,636,000,000.00	2,202,919,681.50	39
		2	Songwe DC	3,150,000,000.00	464,805,666.00	15
		3	Momba DC	1,586,000,000.00	589,067,294.92	37
		4	Mbozi DC	3,047,000,000.00	941,083,088.00	31
		5	Ileje DC	1,403,000,000.00	374,451,830.96	27
			Jumla Ndogo	14,822,000,000	4,572,327,561.38	31
5	Katavi	1	Nsimbo DC	1,191,000,000.00	467,987,996.90	39
		2	Mpimbwe DC	1,608,000,000.00	801,599,715.72	50
		3	Mpanda MC	3,254,000,000.00	949,332,277.17	29

		4	Tanganyika DC	5,565,000,000.00	1,069,157,262.98	19
		5	Mlele DC	957,000,000.00	489,336,954.88	51
			Jumla Ndogo	12,575,000,000	3,777,414,207.65	30
6	Tabora	1	Urambo DC	2,533,000,000.00	700,151,738.24	28
		2	Uyui DC	3,007,000,000.00	884,173,423.27	29
		3	Tabora MC	5,085,000,000.00	1,255,396,328.19	25
		4	Sikonge DC	3,229,000,000.00	758,586,238.21	23
		5	Nzega TC	3,673,000,000.00	683,176,540.99	19
		6	Nzega DC	2,567,000,000.00	603,319,868.80	24
		7	Kaliua DC	3,599,000,000.00	1,746,941,247.00	49
		8	Igunga DC	3,267,000,000.00	1,422,282,722.00	44
			Jumla Ndogo	26,960,000,000	8,054,028,106.70	30
7	Pwani	1	Rufiji DC	3,657,000,000.00	1,512,847,294.48	41
		2	Mkuranga DC	7,826,000,000.00	2,224,978,343.67	28
		3	Mafia DC	1,680,000,000.00	381,737,064.50	23
		4	Kisarawe DC	3,017,000,000.00	870,217,434.22	29
		5	Kibiti DC	2,107,000,000.00	577,200,092.45	27
		6	Kibaha TC	4,491,000,000.00	1,927,031,141.39	43
		7	Kibaha DC	1,886,000,000.00	695,375,343.05	37
		8	Chalinze DC	10,728,000,000.00	2,540,376,723.33	24
		9	Bagamoyo DC	3,914,000,000.00	921,454,248.13	24
			Jumla Ndogo	39,306,000,000	11,651,217,685.22	30
8	Shinyanga	1	Ushetu DC	3,071,000,000.00	762,757,965.60	25
		2	Shinyanga MC	4,043,000,000.00	938,410,529.34	23
		3	Shinyanga DC	2,294,000,000.00	1,044,410,326.00	46
		4	Msalala DC	4,608,000,000.00	1,151,167,714.23	25
		5	Kishapu DC	3,652,000,000.00	696,617,608.47	19
		6	Kahama MC	8,325,000,000.00	2,856,363,889.75	34
			Jumla Ndogo	25,993,000,000	7,449,728,033.39	29
9	Njombe	1	Wanging'ombe D	3,489,000,000.00	763,406,131.82	22
		2	Njombe TC	6,717,000,000.00	1,970,481,326.80	29
		3	Njombe DC	2,982,000,000.00	1,004,868,382.00	34
		4	Makete DC	2,487,000,000.00	798,084,493.44	32
		5	Makambako TC	3,228,000,000.00	781,318,648.31	24
		6	Ludewa DC	2,037,000,000.00	535,005,378.76	26
			Jumla Ndogo	20,940,000,000	5,853,164,361.13	28
10	Iringa	1	Mufindi DC	6,130,000,000.00	2,031,931,164.08	33
		2	Mafinga TC	4,965,000,000.00	1,494,452,299.19	30
		3	Kilolo DC	4,353,000,000.00	976,904,823.00	22

		4	Iringa MC	4,357,000,000.00	1,038,049,823.73	24
		5	Iringa DC	3,882,000,000.00	935,126,214.13	24
			Jumla Ndogo	23,687,000,000	6,476,464,324.13	27
11	Morogoro	1	Ulanga DC	2,432,000,000.00	785,981,315.42	32
		2	Mvomero DC	3,596,000,000.00	588,099,396.13	16
		3	Morogoro MC	11,504,000,000.00	1,926,510,355.14	17
		4	Morogoro DC	3,026,000,000.00	1,364,801,355.18	45
		5	Malinyi DC	2,603,000,000.00	895,096,386.42	34
		6	Kilosa DC	5,240,000,000.00	1,170,944,996.36	22
		7	Mlimba DC	3,367,000,000.00	1,598,667,729.91	47
		8	Ifakara TC	3,927,000,000.00	1,141,968,833.67	29
		9	Gairo DC	1,220,000,000.00	303,930,896.50	25
			Jumla Ndogo	36,915,000,000	9,776,001,264.73	26
12	Mbeya	1	Rungwe DC	5,306,000,000.00	1,623,630,850.00	31
		2	Mbeya DC	4,373,000,000.00	915,742,754.48	21
		3	Mbeya CC	16,610,000,000.00	3,413,533,430.46	21
		4	Mbarali DC	4,790,000,000.00	1,681,365,927.82	35
		5	Kyela DC	3,884,000,000.00	1,006,392,730.49	26
		6	Chunya DC	4,847,000,000.00	1,778,054,346.18	37
		7	Busokelo DC	1,594,000,000.00	520,477,060.03	33
			Jumla Ndogo	41,404,000,000	10,939,197,099.46	26
13	Geita	1	Nyang'hwale DC	1,805,000,000.00	758,989,700.27	42
		2	Mbogwe DC	1,578,000,000.00	617,754,002.00	39
		3	Geita DC	4,668,000,000.00	1,371,923,346.13	29
		4	Geita TC	10,254,000,000.00	2,733,828,041.92	27
		5	Chato DC	3,996,000,000.00	692,418,666.00	17
		6	Bukombe DC	3,162,000,000.00	461,520,481.00	15
			Jumla Ndogo	25,463,000,000	6,636,434,237.32	26
14	Singida	1	Singida MC	4,648,000,000.00	1,204,771,058.65	26
		2	Singida DC	1,357,000,000.00	374,710,837.97	28
		3	Mkalama DC	1,454,000,000.00	484,207,243.05	33
		4	Manyoni DC	2,897,000,000.00	523,687,043.70	18
